JAMHURI YA
MUUNGANO
WA TANZANIA

# UMASKINI KATIKA NGAZI YA WILAYA TANZANIA BARA

Imetolewa na Kamati ya Utafiti na Uchambuzi ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA
Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

## MUHTASARI 2 RIPOTI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA BINADAMU YA MWAKA 2005

**Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Binadamu ya Mwaka 2005 (PHDR) inatoa matokeo ya kazi ya uchambuzi iliyofanyika kwa kutumia mbinu za kuonyesha makadirio ya umaskini wa kipato kiwilaya kwa mara ya kwanza Tanzania. Makadirio haya mapya ya umaskini wa kipato yanaongeza usahihi wa makadirio ya awali, na yakiangaliwa pamoja na taarifa kuhusu viashiria vingine vya ustawi katika ngazi ya wilaya, yanawezesha kutambua mahitaji mahsusi ya watu katika maeneo mbalimbali ya nchi hivyo kuruhusu utoaji wa kipaumbele na mkazo zaidi katika mahitaji hayo. Vilevile kusaidia kuwa na mikakati ya kugawa rasilimali kulingana na mahitaji maalum ya maeneo.**


### Viashiria vya Umaskini kwa Wilaya

Moja ya matokeo muhimu ya na makadirio ya umaskini wa kipato kiwilaya ni kwamba asilimia ya watu waliopo chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi kinatofautiana kwa kiasi kikubwa kati ya mikoa na wilaya.

'Kiwango cha Umaskini' kinatafsiriwa kama asilimia ya watu waliopo chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi. Kwa Tanzania kiwango cha mahitaji ya msingi mnamo mwaka 2000/01 kilikuwa shilingi za Kitanzania 262 kwa kila mtu mzima kwa siku. Ramani na 1 inaonyesha asilimia ya watu wanaoishi chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi Tanzania Bara, kwa wilaya, kwa mwaka 2001. Kutoka katika ramani hii na jedwali linalohusiana na ramani hii lililopo katika ukurasa wa tatu, unaweza kuona kwamba wilaya za Bukoba Mjini, Arusha Mjini, Mbeya Mjini, Mbarali, Morogoro Mjini na Kinondoni zote zina chini ya aslimia 15 ya watu waliopo chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi. Kinyume cha hivyo, katika wilaya za Bunda, Musoma Vijijini, Geita na Serengeti, zaidi ya asilimia 60 ya watu wana kipato chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi.


Taarifa nyingine muhimu ni kwamba wilaya zina viwango tofauti kwa viashiria tofauti vya umaskini. Wilaya yenye alama za juu kwenye kiwango cha moja ya viashiria vya umaskini, siyo lazima iwe na alama za juu kwenye viashiria vingine vya umaskini.

Kwa mfano, baadhi ya wilaya maskini zaidi zimefanya vizuri katika kupunguza viwango vya vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano. Hatahivyo, wilaya ambazo hazifanyi vizuri zimejikusanya katika makundi ya



Asilimia ya watu wanaoishi katika umaskini, kiwilayani kwa mahitaji ya msingi


| | |
|---|---|
| Chini ya 20% | 20.1–30.0 |
| 30.1–40.0 | 40.1–50.0 |
| Zaidi ya 50% | |




Asilimia ya watu walio chini ulingo waumaskini kwa mahitaji ya msingi

| | |
|---|---|
| Za mwisho kumi | Zenye viwango vya chini 11 – 20 |
| Kumi bora | Bora 11 – 20 |
| Katikati | |


Za mwisho kumi | Zenye viwango vya chini 11 – 20 | Katikati | Bora 11 – 20 | Kumi bora




Asilimia ya kaya zinazopata maji kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa



Kiwango cha vifo kwa watoto chini ya miaka mitano



Uandikishaji wa watoto katika shule za msingi wavulana na wasichana



Asilimia ya watu wazima wanaojua kusoma na kuandika

kijiografia; huku wilaya zinazofanya vizuri zaidi zikiwa zimesambaa na nyingi zikiwa katika maeneo ya mijini. Ramani na 2 na jedwali linalohusiana na ramani hii iliyopo kwenye ukurasa wa tatu inaonyesha alama za viashiria vikuu kwa baadhi ya wilaya.

## Kutumia Kanuni kwa Ajili ya Kutenga Bajeti

Taarifa zilizopo kwenye RUMB zinaonyesha kwamba ipo haja ya kutilia mkazo kwenye mahitaji mahsusi ya watu katika maeneo mbalimbali ya nchi. Bajeti ya Serikali ya Tanzania ni zana yenye nguvu ya kuhakikisha kwamba watu wote wanapata huduma sawa za umma na fursa za kiuchumi. Hii inaweza kusaidia kukabiliana na ukosefu wa ulinganifu uliopo (tofauti) kati ya wanaume na wanawake, watu tajiri na maskini, maeneo ya vijijini na mijini, na kati ya maeneo mbalimbali ya nchi. Hatahivyo, Bajeti ya Serikali ni ndogo na inabidi utafiti zaidi ufanyike kuhusu utengaji wa rasilimali.

Gharama ya shughuli za kupunguza umaskini na kuboresha upatikanaji wa huduma zina uwezekano wa kuwa kubwa zaidi kwa wale watu wanaoishi katika maeneo yaliyojitenga. Kwahiyo kutumia utaratibu wa kupanga bajeti inayolingana na kipato cha jumla itamaanisha kwamba watu wachache zaidi watafikiwa katika maeneo yaliyojitenga, na lengo la upatikanaji rasilimali unaolingana halitafikiwa. Utaratibu wa kutenga bajeti kwa ajili ya mamlaka ya mahali husika hivi sasa huzingatia idadi ya watu katika wilaya, umbali wa kwenda kwenye huduma iliyopo karibu (km. shule, zahanati), msongomano wa watu, na asilimia ya watu

## Wilaya zimepangwa kwa Kiwango cha Umasikini wa Kipato, Uandikishaji wa Watoto shuleni Kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5, Watu Wazimu wanaojua kusoma na kuandika na Upatikanaji maji bora

| | Asilimia ya watu walio chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi | | Kiwango cha uandikishaji wa watoto shuleni kwa elimu ya msingi | | Kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano (kwa kila watoto 1,000 walio zaliwa hai | | Kiwango cha watu wazima wanaojua kusoma na kuandika | | Asilimia ya kaya zinazopata maji kutoka mifumo iliyoboreshwa (kutoka kwenye mabomba au vyanzo vilivyoboreshwa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Daraja** | **Wilaya** | **Alama** | **Wilaya** | **Alama** | **Wilay** | **Alama** | **Wilaya** | **Alama** | **Wilaya** | **Alama** |
| ***Ishirini Bora*** | | | | | | | | | | |
| 1 | Bukoba (M) | 11 | Lushoto | 100 | Ngorongoro | 40 | Moshi (M) | 96 | Arusha (M) | 99 |
| 2 | Arusha (M) | 12 | Korogwe | 100 | Monduli | 48 | Arusha (M) | 94 | Nyamagana | 97 |
| 3 | Mbeya (M) | 12 | Muheza | 100 | Arusha (M) | 55 | Ilala MC | 93 | Mbeya (M) | 96 |
| 4 | Mbarali | 13 | Tanga (M) | 100 | Moshi (V) | 57 | Nyamagana | 92 | Mtwara (M) | 96 |
| 5 | Morogoro (M) | 14 | Kibaha | 100 | Simanjiro | 57 | Bukoba (M) | 92 | Rombo | 93 |
| 6 | Kinondoni | 14 | Kisarawe | 100 | Arumeru | 58 | Kinondoni | 92 | Moshi (M) | 92 |
| 7 | Nyamagana | 15 | Karatu | 100 | Moshi (M) | 63 | Iringa (M) | 92 | Kinondoni | 92 |
| 8 | Lushoto | 16 | Mwanga | 100 | Hai | 65 | Mwanga | 91 | Musoma (M) | 92 |
| 9 | Ilala MC | 16 | Same | 100 | Mwanga | 68 | Same | 90 | Kigoma (M) | 89 |
| 10 | Tanga (M) | 17 | Moshi (M) | 100 | Rombo | 73 | Songea (M) | 90 | Temeke | 89 |
| 11 | Bukoba (M) | 17 | Babati | 100 | Same | 84 | Mbeya (M) | 90 | Tanga (M) | 89 |
| 12 | Moshi (M) | 18 | Kigoma (M) | 100 | Babati | 91 | Moshi (V) | 89 | Morogoro (M) | 88 |
| 13 | Arumeru | 18 | Ukerewe | 100 | Karatu | 93 | Temeke | 87 | Arumeru | 85 |
| 14 | Iringa (M) | 18 | Magu | 100 | Nyamagana | 100 | Tanga (M) | 87 | Kyela | 85 |
| 15 | Lindi (M) | 18 | Nyamagana | 100 | Hanang | 103 | Musoma (M) | 87 | Songea (M) | 85 |
| 16 | Kondoa | 21 | Tarime | 100 | Mbeya (M) | 106 | Hai | 86 | Iringa (M) | 85 |
| 17 | Mbozi | 21 | Musoma (V) | 100 | Mbulu | 107 | Morogoro (M) | 85 | Ilala MC | 81 |
| 18 | Hai | 22 | Bunda | 100 | Singida (M) | 108 | Mbinga | 84 | Namtumbo | 79 |
| 19 | Shinyanga (M) | 22 | Musoma (M) | 100 | Kasulu | 109 | Ilemela | 84 | Songea (V) | 77 |
| 20 | Pangani | 22 | Mufindi | 100 | Kondoa | 110 | Songea (V) | 83 | Moshi (V) | 75 |
| ***Ishirini za Mwisho*** | | | | | | | | | | |
| 100 | Singida (M) | 46 | Mpwapwa | 79 | Korogwe | 192 | Ngara | 57 | Mtwara (V) | 26 |
| 101 | Sengerema | 46 | Kilindi | 78 | Kongwa | 195 | Shinyanga (V) | 57 | Kisarawe | 25 |
| 102 | Biharamulo | 48 | Kiteto | 76 | Sumbawanga | 195 | Meatu | 55 | Nzega | 25 |
| 103 | Igunga | 48 | Kilwa | 76 | Newala | 197 | Tandahimba | 54 | Tandahimba | 25 |
| 104 | Bukombe | 48 | Ilemela | 75 | Nachingwea | 198 | Kilindi | 53 | Nachingwea | 25 |
| 105 | Uyui | 48 | Nkansi | 75 | Tandahimba | 200 | Lindi (V) | 53 | Mbulu | 24 |
| 106 | Ukerewe | 48 | Sikonge | 75 | Bukoba (V) | 204 | Bukombe | 53 | Kiteto | 23 |
| 107 | Manyoni | 49 | Dodoma (M) | 75 | Tarime | 207 | Kilwa | 52 | Lindi (V) | 23 |
| 108 | Hanang | 49 | Kisulu | 74 | Morogoro(V) | 209 | Dodoma (V) | 52 | Tarime | 22 |
| 109 | Mbulu | 49 | Simanjiro | 72 | Ngara | 212 | Bariadi | 51 | Kilwa | 22 |
| 110 | Babati | 50 | Kongwa | 72 | Tunduru | 212 | Rufiji | 51 | Rufiji | 21 |
| 111 | Kisarawe | 51 | Ngorongoro | 71 | Namtumbo | 213 | Igunga | 49 | Mafia | 17 |
| 112 | Lindi (V) | 51 | Monduli | 71 | Mpwapwa | 217 | Uyui | 49 | Musoma (V) | 17 |
| 113 | Meatu | 53 | Urambo | 69 | Kilwa | 217 | Nzega | 49 | Liwale | 16 |
| 114 | Namtumbo | 55 | Ulanga | 68 | Lindi (V) | 220 | Sikonge | 49 | Urambo | 14 |
| 115 | Singida (V) | 56 | Igunga | 67 | Liwale | 221 | Mkuranga | 47 | Kishapu | 13 |
| 116 | Serengeti | 61 | Dodoma (V) | 66 | Masasi | 225 | Mtwara (V) | 46 | Uyui | 11 |
| 117 | Geita | 62 | Nzega | 65 | Mtwara (V) | 231 | Monduli | 43 | Igunga | 9 |
| 118 | Musoma (V) | 64 | Kibondo | 63 | Dodoma (V) | 239 | Kiteto | 42 | Mkuranga | 9 |
| 119 | Bunda | 68 | Uyui | 58 | Rwangwa | 250 | Ngorongoro | 28 | Sikonge | 7 |

Ufunuo: **M** = Mjini **V** = Vijijini

*Chanzo: Kilama na Lindeboom (tazama hapa chini), kwa kutumia Sensa ya wat na ya Makzi ya mwaka 2005, idaraya Takwimu mwaka 2003, Takwimu za Msingi za Wizara ya Elimu za mwaka 2004*

ambao ni maskini, katika juhudi ya kupunguza baadhi ya vipengele vinavyoweza kuzuia kuwepo kwa uwiano sawa katika ugawaji wa rasilimali.

Matokeo yaliyotokana na uchambuzi wa makadirio ya umaskini wa kipato unaonyesha kwamba kanuni hizi zipo katika mwelekeo sahihi. Kwahiyo, utumiaji thabiti wa kanuni hizi unahitajika, ili kusaidia mikakati ya kugawa wa rasilimali. Matokeo yanayotokana na makadirio ya umaskini wa kipato yanaweza pia kusaidia kuboresha kanuni hizi na kuendeleza matumizi yake kwa kutumia taarifa mahsusi zinazoaminika katika ngazi ya wilaya.

## Vidokezi na Changamoto

- Wilaya nyingi zina mahitaji tofauti kutoka kwa sekta mbalimbali. Uchambuzi wa makadirio ya umaskini unaweza kusaidia kuweka wazi maeneo yanayohitaji kipaumbele kutoka kwa sekta mbalimbali na pia kwa ajili ya kuleta uwiano katika mgawanyo wa rasilimali za fedha na watu.

- Kwa kuwa serikali kuu imekuwa ikitenga fedha nyingi zaidi kwa serikali za mita, hivyo basi inalazimu kuimarisha ujuzi wa usimamizi wa matumizi wa fedha wa serikali za mita.

- Taarifa zinazotokana na makadirio ya umaskini kiwilaya zinaweza kutumika kuelezea tofauti za kijiografia katika utendaji wa vipengele tofauti vya umaskini kwa watu wengine zaidi. Mbinu hii pia itasadia kuelewa mahitaji maalum ya wilaya na hivyo kuweza kuwepo kwa jitihada zaidi kushugulikia masuala hayo.

## Maelezo Kuhusu Njia Iliyotumika na Taarifa za Ziada

Mbinu za kuonyeshaji makadirio ya umaskini wa kipato iliyotumika katika uchambuzi huu iliunganisha taarifa kutoka katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2000/01 na makadirio ya viwango vya kipato vya kaya na uwiano wa kaya zinazoishi chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi kwa kila wilaya.

Taarifa kamili ya PHDR ya mwaka 2005 imetolewa katika jedwali na katika ramani zinazoonyesha mgawanyo wa viashiria tofauti vya umaskini katika mikoa 22 na wilaya 119. Hii inaweza kuwa zana muhimu katika utungaji sera na upangaji mipango kwa kutumia ushahidi. Ramani hizi zinaonyesha sifa-bainifu mbalimbali za wilaya katika kuelezea viashiria tofauti vya umaskini. Zinaweza pia kufanya ukosefu wa uwiano kijiografia ufikiriwe kwa undani zaidi na kutolewa maelezo ya kina.

Maelezo zaidi ya uafiti wa umaskini katika ngazi ya wilaya umeelezwa katika kitabu kilechoandikwa na Blandina Kilama na Wietze Lindeboom na wenzake "Where are the Poor in Tanzania?" yaani, "Maskini wako wapi nchini Tanzania?" Njia hii imetokana na chapisho lililoandikwa na Elbers, Lanjouw J. C. na Lanjouw, P (2003) linaloitwa Micro-level estimation of Poverty and Inequality; Econometrica, Econometric Society, Vol 71(1), uk. 355 hadi 364.

Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2005 inatoa taarifa muhimu kuhusu viwango na mwelekeo wa umaskini nchini Tanzania, ikilinganisha na malengo kutoka katika Malengo ya Milenia ya Maendeleo, Mkakati wa Kutokomeza Umaskini (MKU) na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Ripoti hii inapatikana katika nakala pepe, na ripoti iliyochapishwa inaweza kupatika kutoka:

**Idara ya Kuondoa Umaskini, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Dar es Salaam.**

Simu:(022) 2113856 / 2124107

Barua pepe: mkukutamonitoring@gmail.com

Anwani ya tovuti: http://www.tanzania.go.tz/poverty/index.html/

na kutoka **REPOA (Research on Poverty Alleviation)**

Simu: (022) 2700083

Barua pepe: repoa@repoa.or.tz

Anwani ya tovuti: http://www.repoa.or.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA